VIGEZO NA MASHARTI YA KADI YA SPICE

1.TAFSIRI YA MANENO

- ATM' itamaanisha mashine ya kuchukulia pesa inayojiendesha wenyewe.
- Kadi ya SPICE na Kadi inamaanisha kadi ya ATM iliyotolewa na Benki ya Watu wa Zanzibar.
- Matumizi ya kadi itamaanisha pesa zilizotolewa kwa kutumia kadi ya SPICE. PBZ itamaanisha Benki ya Watu wa Zanzibar.
- "PIN" itamaanisha namba ya siri ya utambulisho itakayokabidhiwa kwa mmiliki kwa matumizi ya kadi yake.
- Mmiliki wa kadi itamaanisha mtu aliyepewa kadi ya SPICE, ambaye akaunti yake itapungua kulingana na matumizi ya kadi yake.
- "Akaunti yako" inamaanisha akaunti yako ya Benki ya Watu wa Zanzibar ambayo itakuwezesha kupata kadi ya SPICE.

2.MADHUMUNI NA MATUMIZI YA KADI YA SPICE

2.1 Kila SPICE kadi itakuwa kwa matumizi ya mmiliki wa kadi tu.

2.2 Kadi ya PSICE itakuwezesha kutoa fedha kutoka kwenye ATM yoyote ya PBZ au ATM ambazo zilizoainishwa au zitakazoanishwa katika siku za baadae.

2.3 Kadi ya SPICE pia itakuwezesha kujua salio lako pia kupata taarifa fupi ya salio lako katika na maaelezo ya matumizi ya kadi yako ya karibuni zaidi.

2.4 Kadi ya SPICE itakuwezesha kubadilisha namba yako ya siri kwenye ATM yoyote ya PBZ au katika kituo cha ATM cha PBZ.

3.UTOWAJI WA KADI YA SPICE KWA MTEJA

3.1 PBZ itatoa kadi ya SPICE kwa mteja yoyote ambaye anayo akaunti ya akiba au ya biashara ya PBZ na baada ya kupokea fomu ya maombi ya kadi ya SPICE iiyojazwa na kusainiwa

3.2 PBZ itatoa kadi kwa akaunti ya ushirika watakapohitaji na baada ya pande zote kujaza mkataba, na ni kadi moja tu watakayopewa.

4.MAJUKUMU YA MMILIKI WA KADI YA SPICE

4.1 Mmiliki wa kadi anajukumu la kuhakikisha usahihi wa maelezo wa malipo yote ambayo yatafanywa katika ATM na PBZ haitochukuwa jukumu lolote kutokana na hayo.

4.2 Mmiliki wa kadi atakuwa na jukumu la uangalifu na kuchukuwa tahadhari juu ya ya usalama wa kadi ya SPICE na kuhakikisha kuwa kadi haitumiki kwa matumizi yasiyo ya halali au kutumika isivyokusudiwa.

4.3 Mmiliki wa Kadi achukuwe tahadhari ya namba yake ya siri na asiandike katika kadi yake ambayo maandiko hayo au kadi yake inaweza kupotea, kuibiwa au kunakiliwa.

5.JINSI YA KADI YA SPICE INAVYOFANYA KAZI

5.1 Mmiliki wa kadi atatakiwa kulipa gharama zote za utendaji ili kumuwezesha mteja kupatiwa kadi yake. Benki itakuwa na uwezo wa kubadilisha gharama hizo wakati wowote. Taarifa itatolewa kabla ya mabaliliko yoyote.

5.2 PBZ itapunguza fedha kulingana na kiasi cha fedha kitakachotolewa na kurikodiwa na ATM kama mmiliki wa kadi alivyotumia, kiasi hicho kitapunguzwa kutoka kwenye akaunti ya mmiliki.

5.3 Kiasi cha juu cha fedha utakazoweza kutoa kwa kutumia kadi ya SPICE ni TZS. 400,000.00 (Shilingi za kitanzania) kwa siku.

5.4 Mmiliki wa kadi na mmiliki wa akaunti wanakiri kuwa PBZ ina haki ya kuweka kikomo cha kiasi cha kutoa fedha pamoja na kiasi cha kuhamisha fedha kutoka akaunti moja kwenda nyingine.

5.5 Mmiliki wa kadi anaweza kutozwa kiasi cha fedha, kila atakapotumia kadi ya ATM.

5.6 Matumizi yasiyo sahihi ya ATM au kutumia namba ya siri pasi na mafanikio mara tatu mfululizo itapelekea kukwama kwa kadi yako ambapo mmiliki wa kadi ataweza kupata kadi yake kwa kupiga simu katika tawi la PBZ au kwa kuenda mwenyewe katika tawi lililo karibu nawe pamoja na vielelezo vyako vinavyokutambulisha.

5.7 Kadi ya SPICE haitotumiwa na akaunti ya kikundi chochote..

5.8 Muombaji wa kadi lazima awe na umri usiopungua miaka 18 au zaidi.

5.9 PBZ haitawajibika kutokana na kushindwa kufanya kazi, kucheleweshwa au kuharibika kwa kifaa chochote cha mfumo wa unendeshaji mtandao, upotevu au uharibifu utakao mpata mmiliki wa kadi.

5.10 Kiasi cha fedha kitakachotolewa na kurekodiwa na ATM, kama ilivyotumiwa na mmiliki wa kadi, kitapunguzwa kutoka akunti ya mmiliki wa akaunti.

5.11 Mmiliki wa kadi asitumie mpaka akazidisha kiwango cha juu cha fedha anachoruhusiwa kuchukuwa pale akaunti ya akiba inaporuhusiwa.
Riba itatozwa kawkenye kiasi chochote kilichozidishwa kutolewa bila ya kujali aina ya akaunti kwa kujumlishwa na kiasi kilichotolewa.
Riba itatakiwa kulipwa mara itakapodaiwa kwa kiasi cha 25% kwa mwaka.

5.12 Kadi ya SPICE itatumika mpaka itapokwisha muda wake, au itaposimamishwa matumizi yake na PBZ hadi itakapo patiwa kadi nyengine.

5.13 Kadi ya SPICE itatumika ndani ya mipaka ya Jmhuri ya Muungano wa Tanzania tu.

5.14 Kadi ya SPICE itaweza kubadiliswa baada ya kwisha muda wake ikiwa PBZ itaridhika na matumizi na utunzaji wa SPICE kadi, isipokuwa kama mteja atatoa taarifa ya kughairisha.

5.15 Kadi ya SPICE itatoa fedha katika akaunti za ATM zilizokusudiwa maalumu na si kwenye akaunti nyengine yoyote.

5.16 Kadi ya SPICE inauwezo wa kutoa fedha za Kitanzania tu.

5.17 Ikiwa mmiliki wa kadi atasita kuhoji matumizi yaliyoonyeshwa kwenye ankara yake ndani ya siku 14 kutoka tarehe iliyoonyeshwa kwenye ankara yake, ya matumizi atahesabika kuwa amekubaliana na uwajibikaji wake kwa malipo hayo kulikofanywa na PBZ.

5.18 Inapotokea akaunti kufungwa, ni jukumu la mmiliki wa kadi kurejesha kadi mara moja PBZ.

6. KUPOTEA/KUIBIWA KADI, MATUMIZI YASIO SAHIHI AU KUKIUKA MASHARTI YA USALAMA

6.1 Ikiwa kadi itapotea, kuibiwa au kumilikiwa na mtu asiyehusika au namba ya siri kujulikana na asiyehusika, mmiliki wa kadi lazima achukuwe hatua ya kusimamisha matumizi ya kadi yake au abalilishe namba yake ya siri kwa kuwasiliana na meneja wa tawi lolote la PBZ wakati wa kazi.

6.2 Taarifa ya kupotea au kuibiwa kwa kadi haitakuwa na nguvu mpaka itakapothibitishwa kwa maandishi na mmiliki wa kadi ndani ya siku mbili za kazi.

6.3 Ikiwa taarifa za upotevu wa kadi zitatolewa na mtu aliyeruhusiwa au asiyekuwa mmilikiwa kadi. PBZ haitahusishwa na matokeo ya uharibifu utakao mtokea mmiliki wa kadi.

6.4 Kubalilisha kadi iliyopotea au kuibiwa utafanywa kwa malipo. Gharama itakuwa kama zilivyopangwa na PBZ.

7.MAELEZO MAALUMU KUHUSIANA NA UENDESHAJI WA ATM

7.1 Mmiliki wa akaunti anaelewa kuwa matumizi ya namba ya siri/sahihi yanamwezesha mtumiaji kutumia akaunti na kupata taarifa zinazohusiana na matumizi ya akaunti na kufahamu hivyo mmiliki wa akaunti anaondoa madai au malalamiko yoyote kwa PBZ yanayotokana na mmiliki kadi kuhusiana na matumizi ya kadi hiyo.

7.2 Kadi itabadilishwa kwa uamuzi wa PBZ wakati muda wa matumizi utakapokwisha, au maelezo tofauti yatakayotolewa na mmiliki kadi, pia kadi inaweza kusitishwa uhalali wake wakati wowote au kukataa kuongeza muda wa matumizi baada ya kwisha bila sababu zozote.
Pindi ikitokea hivyo mmiliki kadi hatasikilizwa malalamiko yoyote yatakayotolewa kutoka kwake na hayatakuwa na nguvu.

7.3 Benki inahaki muda wote kuingiza masharti mapya au kubadilisha masharti yaliyokuwepo sasa . mmiliki wa kadi atalazimika kukubaliana na masharti mapya yatakayo pendekezwa na PBZ, wakati mmiliki wa kadi atapokuwa amepata maelekezo hayo kwa njia yoyote ambayo PBZ itaoneleya ndiyo bora.

7.4 Kwa muda wote kadi itabakia mali ya PBZ, ambayo kwa uamuzi wake inaweza kusitisha uhalali wakati wowote au kukataa kuengeza muda wa matumizi baada ya kwisha bila kutoa sababu zozote, ikitokea hivyo mmiliki wa kadi atatakiwa kusitisha matumizi ya kadi hiyo, mmiliki wa kadi.
Mmiliki wa kadi atakabiliwa na mashtaka iwapo ataendelea na matumizi ya kadi hiyo.

7.5 Mmiliki wa kadi na mmiliki wa akaunti wanakubali kuwa fomu itakayotolewa na meneja yoyote wa benki ya PBZ itakuwa ni ushahidi kamili kuhusiana na kiwango cha fedha alichonacho mmiliki wa akaunti wa PBZ na kwamba matumizi ya fedha yanaweza kufanywa kwa kutumia namba ya siri ya mmiliki wa kadi na si vyenginevyo.

8.MAAMUZI YA KORTI

8.1 Matumizi yasiyosahihi ya kadi au udaganyifu wowote utakaopelekea mmiliki wa kadi kutoa fedha, itapelekea kuzuiliwa kadi yake na kufunguliwa mashtaka.

8.2 Benki itakuwa na haki, kutafuta taarifa binafsi za mmiliki wa kadi kwa benki ya biashara au taasisi yoyote ya fedha, ikiwa kutakuwa na matumizi ya kadi ya udanganyifu yatakayofanywa na mmiliki wa kadi. Au mmiliki wa kadi atawajibika kwa benki kutoa taarifa juu ya wizi, upotevu,au shutuma za wizi kwa ukamilifu ili kuweza kusaidia upatikana wa taarifa hizo.

8.3 PBZ inaweza kutoa taarifa zinazaohusu mmiliki wa akaunti kwa mtu yoyote kwa madhumuni ya kuzuia udanganyifu au vyenginevyo ambao utahusisha taarifa za kibenki kuhusiana na akaunti yake. Pia PBZ haitaweza kutoa taarifa za mmiliki wa kadi isipokuwa kwa wakala wetu, isipokuwa tutakapolazimika kwa mujibu wa sheria.

8.4 Endapo PBZ itafungua kesi yoyote dhidi ya mmiliki wa kadi na mmiliki wa akaunti, wahusika hao watalazimika kulipia gharama zote za kuendeshea kesi itakayofunguliwa dhidi yao na PBZ.

8.5 Mashitaka yoyote yatayofunguliwa Kortini ili kuwezesha kurejeshwa pesa zilizochukuliwa kwa njia isiyohalali, taarifa za kibenki kuhusu matumizi ya kadi kuchukua pesa pamoja na nakala zake zilizothibitishwa zitatumika kama ushahidi tosha mahakamani kuendeshea mashtaka yoyote yatakayofunguliwa ili kurejesha pesa zinazohusiana na matumizi ya kadi.

8.6 Ikiwa mmiliki wa kadi atafariki, kufilisika au kukiuka kipengele chochote cha mkataba huu, PBZ mbali ya kuchukuwa hatua zinazofaa zikiwa pamoja na zilizokuwemo katika mkataba huu kadri itakavyokuwa na ulazima wa kuzuia matumizi yoyote ya kadi ya SPICE kuchukua pesa.

8.7 Mmiliki wa kadi atawajibika kuitunza na kuitumia Kadi kwa mujibu wa vigezo na masharti pamoja na maelezo yote yatakayotolewa na PBZ.

8.8 Mkataba huu, pamoja na masharti na vigezo vya matumizi na maelekezo ya uendeshaji mashine za kutolea pesa vitasimamiwa na kutafsiriwa kwa mujibu wa sheria za Zanzibar.